JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI ISIMILA

Namba za Simu
Mkuu wa Shule: 0753 080 790
Makamu Mkuu wa Shule: 0755 683 093
Matron: 0752 001 408

S.L.P. 1459,
IRINGA.

Kumb. Na. ISS/ADM/2020/06 12/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI……..…….…….
SHULE YA MSINGI ……
IRINGA.

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISIMILA MWAKA 2021 WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA.</u>

1.0 **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Isimila ipo umbali wa km 40 Kusini mwa mji wa Iringa, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 **SARE YA SHULE**

1. Blauzi/shati mbili (2) tetron nyeupe mikono mifupi (nusu kanzu kwa Waislamu wa kike).

2. Suruali mbili kwa wavulana na sketi mbili (2) zenye marinda madogo ya kawaida kwa wasichana au suruali isiyobana kwa Waislamu na hijabu nyeupe isiyo na urembo. (Rangi ya kitambaa cha shati na suruali imeambatanishwa).

3. Jozi mbili za viatu vyeusi visivyo na kisigino vya **kufunga** na **kamba.**

4. Jozi mbili za soksi nyeupe.

5. Sweta ya rangi ya bluu yenye “V” shingoni isiyopasuliwa mbele.

6. Raba jozi mbili kwa ajili ya muichezo

7. Nguop za michezo Traki suti ya bluu bahari

8. Nguo ya kazi (shamba dress) tetron nzito rangi ya light blue na suruali nyeusi kwa wavulana.

9. Daftari 10 counter books pamoja na karatasi nyeupe A4 za kufanyia mazoezi, kalamu na mkebe wa hesabu.

10. Shule hii ni ya kutwa, hivyo mzazi utagharamia chakula, nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia mimgozi yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoljia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzinghatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

(iv) Kuwahi, kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(ix) Kutunza mali za umma

(x) Kusimama na kumsalimia Mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo.

(xi) Kutumia lugha nzuri wakati wote.

(xii) Kushirikiana na kusaidiana na mwanafunzi wengine katika kazi.

(xiii) Kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mkuu anayekuita

(xiv) Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa vyama na serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.

(xv) Kukaa kimya darasani na kutoka kwa ruhusa ya Mwalimu au kiongozi aliyeko darasani.

(xvi) Mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na nje ya shule.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(a) Wizi

(b) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi kubeli, sigara n.k.

(e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au na mtu yeyote yule.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.

(h) Kudharau Bendera ya Taifa

(i) Kupata ujauzito, kutoa mimba au kusababisha mimba

(j) Kukataa adhabu kwa makusudi

(k) Utoro wa shule wa muda mrefu

(l) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(m) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(n) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(o) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(p) Kutembelea nyumba za walimu, Ofisi ya Mkuu wa Shule pamoja na ofisi ya walimu bila ruhusa au sababu ya msingi.

(q) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au line ya simu katika mazingira ya shule.

(r) Kudharau Bendera ya Taifa

(s) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa simu n.k.

(t) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4.0 **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

(a) Medical Examination Form, ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukubaliana na sheria, kanuni na maenelezo mengine yatakayotolewa na shule.

Ni matumaini yangu kuwa utatumia vizuri nafasi hii na kwamba utatumia **JUHUDI** na **MAARIFA** ya hali ya juu ili uweze kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, usafi na michezo.

Shule ya Sekondari Isimila ni shule ya kutwa. Shule ipo umbali wa Km 26 kutoka Iringa Mjini na Km 10 kutoka barabara kuu iendayo Mbeya upande wa Mashariki (Sehemu iitwayo Wenda au Njiapanda ya Mlolo). Shule itafunguliwa tarehe 11/1/2021

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Isimila Sekondari.

.....
FRANK MAHENGE
MKUU WA SHULE
ISIMILA SEKONDARI